BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Kwanza – Tarehe 6 Februari, 2019.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 7 Disemba, 2018.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2018 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2018 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

III. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

32. MHESHIMIWA MOHAMED SAID MOHAMED (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Tarehe 1 hadi 6 Oktoba, 2018 nchi ya Korea ya Kusini, kulifanyika mkutano unaohusiana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani wanasayansi zaidi ya 500 kutoka katika nchi zaidi ya 130 walihudhuria. Miongoni mwa ajenda zilizojadiliwa ni kuongezeka kwa kina cha bahari kinachosababishwa na kuongezeka kwa joto duaniani "*Global warming"*.

(a) Je, Serikali kwa kiwango gani inafuatilia mikutano kama hii ya kitaalamu ambayo ripoti zake zinaweza kutupa sura nzima ya tatizo tunalokabiliana nalo.

(b) Kwa kuwa athari za kuongezeka kwa kina cha maji zimeshaanza kujitokeza Zanzibar katika maeneo mbali mbali, Je, Serikali imeshachukua hatua gani na imejipangaje kwa siku za baadae kukabiliana na janga hili.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

39. MHESHIMIWA TATU MOHAMED USSI (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Kuna baadhi ya Shirika/Taasisi za Umma wanatoa matangazo ya kazi kwa kuangalia sifa za kielimu pamoja na uzoefu wa miaka 3, 5 au 10. Sharti hilo huwakosesha ajira vijana wetu waliomaliza masomo yao kwa kukosa uzoefu wa kazi.

(a) Je, Shirika/Taasisi za Umma hizo hazioni kuwa zinavunja moyo vijana ambao wana sifa zote lakini wamekosa sifa hiyo ya uzoefu.

(b) Je, Shirika/Taasisi za Umma zinaonaje kuajiri vijana hao ili wakapata uzoefu wakiwa wanaendelea na kazi.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

23. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikifanya juhudi ya kuwashauri wamiliki wa hoteli za kitalii na uwekezaji mwengine hapa nchini kuwatumia wakala wa Ulinzi (JKU) badala ya kutumia “watchmen” na CCTV Camera pekee.

(a) Je, ni hoteli ngapi za kitalii nchini ambazo wameshatekeleza ushauri huo.

(b) Je, hatua gani kwa hoteli ambazo hadi sasa hazijafuata ushauri huo na zinahatarisha maisha ya wageni wetu na mali zao dhidi ya wahalifu wanaoibuka siku hadi siku.

35. MHESHIMIWA HIDAYA ALI MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kulikuwa na kadhia ya soko la Mwanakwerekwe kuhamishwa Manispaa ya Mjini kwenda Manispaa ya Magharibi “B”. Hata hivyo, kuna taarifa kuwa baada ya siku 10 soko hilo limerudi tena Manispaa ya Mjini.

(a) Je, kadhia hii ya uhamisho ilifanywa na nani.

(b) Je pesa zilizokusanywa na Manispaa ya Magharibi “B” watarejeshewa wenyewe Manispaa ya Mjini.

(c) Kutokana na changamoto iliyopo njia ya kuingilia ndani sokoni kwa njia ya magari, Je, hamuoni kwamba kuna haja ya kuitengeneza ili iwe salama kwa wananchi na waondokane na usumbufu unaotokana na njia ile.

Wizara ya Elimu Na Mafunzo ya Amali:

27. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa jitihada zinachukuliwa na wawekezaji katika skuli binafsi kwa kusaidia uendelezaji wa elimu nchini. Na kwa kuwa Wizara ya Elimu inazitaka skuli binafsi kufuata Mtaala mmoja kwa skuli za Serikali na binafsi,

Je, Wizara inazisaidia vipi skuli za binafsi juu ya matatizo ya ukosefu wa vitabu vya kusomea.

Wizara ya Fedha na Mipango:

22. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ni mali ya wananchi wa Zanzibar na hivyo wananchi wanaitegemea benki hiyo ijiendeshe kibiashara na kupata faida ili wananchi waweze kunufaika kupitia benki hiyo.

(a) Je, ni yepi masharti na vigezo ambavyo vinahitajika ili mjasiriamali mdogo na mkulima aweze kupata mkopo ambao utamkwamua katika biashara zake na kujiendeleza kwa kilimo au uvuvi.

(b) Je, kwa mwaka 2017/2018 hadi kufikia mwezi Oktoba, 2018 ni wajasiriamali wangapi ambao PBZ imewakopesha kwa ajili ya kuwawezesha na kujiendeleza kibiashara.

Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

40. MHESHIMIWA TATU MOHAMED USSI (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Katika kijiji cha Mgagadu kulikuwa na sehemu ya kihistoria (pango), ambalo lilikuwa na minyororo iliyokuwa wakifungwa na kuingizwa watumwa katika pango hilo. Katika sehemu

hiyo wananchi na wanafunzi walikuwa wanakwenda kujifunza historia ya nchi yao.

(a) Je, Wizara inalijua hilo.

(b) Je, Wizara yako imechukua hatua gani kuliimarisha eneo hilo ili wananchi wetu waendelee kujifunza historia ya nchi yao.

71. MHESHIIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Idara Mambo ya Kale, ina jukumu la kuhifadhi mambo ya kale yanayotokana na maumbile ya kudura ya M/Mungu na yapo mambo ambayo yametengenezwa na binadamu ikiwemo miti mikubwa na ya muda mrefu lakini bado sijaona uwekaji wa kumbukumbu wa vitu kama hivyo. Aidha kuna maeneo ya miujiza na majengo ya kale huwa hatuna utamaduni wa kuweka kumbukumbu na kuyatunza maeneo kama hayo.

(a) Je, Serikali imeshafanya utambuzi wa maeneo yote ya kale yenye kuweza kutuletea utalii wa vivutio kama hivyo.

(b) Kama Serikali ishafanya utambuzi huo, Je, ni maeneo mangapi yaliyokubalika kuwa ni vivutio vya kitalii.

(c) Je, ni maeneo gani hayo yaliyokubaliwa.

<u>Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:</u>

50. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Jengo linalotumika kwa ajili ya Mahakama ya Ardhi liliyopo Majestic Vuga ni chakavu na lenye kuhitaji matengenezo makubwa sambamba na jengo la Mahkama ya Ardhi Mkoa wa Kaskazini Unguja liliyopo Gamba. Majengo haya yanahitaji kuangaliwa kwa namna yake ili yaweze kutumika yakiwa kwenye hali salama kwa wafanyakazi wa Idara hiyo.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kinahitajika ili kuweza kufanikisha matengenezo ya majengo hayo.

(b) Je, hadi kufikia mwezi Oktoba, 2018, Wizara imepata kiasi gani cha fedha kwa ajili ya matengenezo ya majengo hayo.

(c) Je, kuna mpango gani mbadala ambao unaweza kufanyika kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kama Wizara husika itashindwa kupata fedha za matengenezo kwa ajili ya kuyahami majengo hayo.

Wizara ya Afya:

34. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa wananchi wa kijiji cha Mpapa wameamua kuanza kujenga kituo cha afya ili kuwapunguzia shida ya matibabu wananchi hao.

Na kwa kuwa kituo hicho kikimalizika vijiji vya jirani vyote kama vile Pagali, Vilima viwili Dunga njia nne, Mzuri hendi, Panga nguruwe na Mpapa watafaidika na huduma hiyo.

Je, ni lini Wizara yako itakimaliza kituo hicho ili kuwapunguzia kero ya afya wananchi hao.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

28. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kutokana na kuongezeka kwa watu wanaotumia vyombo vya usafiri wa baharini kama vile boti kwa ajili ya usafiri, kutoka Dar es Salaam hadi Zanzibar.

Je, ni utaratibu upi unaotumika kuhakikisha tunakuwa na ulinzi na usalama wa abiria ndani ya vyombo hivyo.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

11. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Serikali yetu imejitahidi kuhamasisha wakulima wa mazao mbali mbali ambapo wananchi wameitikia wito na kuingia kwa wingi katika ukulima wa mazao hasa tungule na mboga mboga. Hata hivyo, sasa kumejitokeza tatizo la soko na kuanguka kwa bei kwa mazao kama tungule.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kila zao lenye nguvu ya kuzaliwa sana Zanzibar linapata soko au viwanda vya kusindika mazao hayo yasiharibike.

(b) Je, Serikali haioni umefika wakati sasa wa kupata viwanda vidogo vidogo vya matunda na “juice” zinazotoka Zanzibar ambazo zina uhalisia wa matunda hayo.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Mwanasheria Mkuu wa Serikali:

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2018 na mambo mengine yanayohusiana na hayo. - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
6 Februari, 2019.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.